


Tom muuza ndizi



- ✎ Humphreys Odunga
- ✉ Zablon Alex Nguvu
- 📄 Matteo E. Mwita
- || 2
- 🗨️ Kiswahili! SW



Global Storybooks

globalstorybooks.net

Tom muuza ndizi

- ✎ Humphreys Odunga
- ✉ Zablon Alex Nguvu
- 📄 Matteo E. Mwita



This work is licensed under a Creative Commons Attribution 4.0 International License.
<https://creativecommons.org/licenses/by/4.0>





Tom anabeba tenga la ndizi
zilizoiva.

Tom anaenda sokoni kuuza
ndizi.






Sokoni watu wananunua
matunda.





Tom anajitwisha tenga
kichwani na kwenda nyumbani.

Lakini hakuna anayenunua
ndizi za Tom. Wanapenda
kununua matunda kutoka kwa
akina mama.



Tom ananunua sabuni, sukari,
na mkate. Anaweka vitu
kwenye tenge lake.







“Kwenye jamii yetu, ni wanawake pekee ndio wanaouza matunda,” watu wanasema. “Ni mwanamume wa aina gani huyu?” watu wanahoji.




Mara, tenga linakuwa tupu. Tom anahesabu pesa alizopata.



Lakini Tom hakati tamaa.
Anaita, "Nunua ndizi zangu;
Nunueni ndizi zangu tamu
zilizoiva!"



Watu wengine wanakuja
kwenye kichanja. Wanunua
ndizi za Tom na kuzila.



Mwanamke mmoja anachukua kichane cha ndizi kutoka kwenye tenga. Anaziangalia ndizi kwa umakini.



Mwanamke ananunua ndizi.